# Wanandoa Kama Wewe na Mimi

*Masomo Kutoka Kwa Maisha Ya Wanandoa Kumi Na Wawili Katika Biblia*

**F. Wayne Mac Leod**

Light To My Path Book Distribution
Sydney Mines, Nova Scotia CANADA

Wanandoa Kama Wewe na Mimi

Hakimiliki © 2019 ya F. Wayne Mac Leod

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya kitabu hiki inaweza kunakiliwa au kusambazwa kwa namna yoyote au njia yoyote ile bila idhini ya maandishi ya mwandishi.

Nukuu za maando zilezowekwa alama (NIV) zimechukuliwa kwenye biblia,Toleo jipya la kimataifa®, NIV®. Hakimiliki © 1973, 1978, 1984, 2011 ya Biblica, Inc.™ kutumiwa kwa ruhusa ya Zondervan. Hakizote zimehifadhiwa duniani kwetu. . www.zondervan.com The “NIV” na “Toleo jipya la kimataifa” ni chapa za biashara zilizo sajiliwa na hati miliki ya marekani na ofisi -ya chapa za biashara za Biblia, Inc.™

Nukuu za maandiko zilizowekwa alama (ESV) zimetoka kwenye ESV ® Biblia (Biblia takatifu, toleo la kawaida la kingereza®), hakimiliki © 2001 na kupitia, huduma ya uchapishaji ya wahubiri wa habari njema. Zimetumika kwa ruhusa haki zote zimehifadhiwa.”

Nukuu za maandiko zilizowekwa alama (NLT) zimechukuliwa katika Biblia takatifu, tafsiri mpya hai, hakimiliki ©1996, 2004, 2015 ya Msingi wa Nyumba ya Tyndale. Imetumiwa kwa ruhusa ya Nyumba ya Tyndale wachapishaji, Inc., Carol Stream, Illinois 60188.haki zote zimehifadhiwa.

Nukuu ya maandiko kutoka toleo lililoidhinishwa la (King James). Haki katika toleo lililoidhinishwa nchini Uingereza zimekabidhiwa taji. Imetolewa tena kwa idhini yay a mwenye hati miliki ya taji, Chuo cha Cambridge.

# Yaliyomo


Dibaji ..................................................5

1 - Adamu na Hawa: ..................................................7

2 - Ibrahimu na Sara: ..................................................11

3 - Lutu na Mkewe: ..................................................19

4 - Isaka na Rebeka: ..................................................25

5 - Yakobo na Lea: ..................................................31

6 - Musa na Sipora: ..................................................37

7 - Daudi Na Wake Zake: ..................................................43

8 - Sulemani Na Wake Zake: ..................................................51

9 - Boazi na Ruthu: ..................................................57

10 - Samsoni na Mwanamke wa Timna: ..................................................61

11 - Manabii Na Wake Zao: ..................................................67

12 - Akila na Prisila: ..................................................73

Light To My Path Book Distribution ..................................................77

# Dibaji

Wote tunavutiwa na kile tunacho kiona kikituzunguka. Dhana yetu ya wanandoa bora ilitoka kwenye sehemu ya kile tukionacho kwenye mahusiano mengine. Katika somo hili, tutaangalia wanandoa kumi na wawili katika Biblia. Walikuwa wanandoa kama wewe na mimi. Walipata majaribu kama wewe na mimi. Wengine walifanikiwa kuyashinda majaribu. Wengine wakawa mawindo yao. Lengo la mifano hii kumi na mbili ni kukutia moyo katika ndoa yako. Utaona hatari za kuzikwepa na kuona mifano ya kufata. Kitu cha muhimu ni kumwacha Bwana akuongoze kupitia vielelezo ya Biblia. Ipo kwaajili ya maelekozo yako na kukutia moyo. Na mafundisho haya rahisi yakutie moyo katika maisha yako kama mwanandoa.

F. Wayne Mac Leod

# 1 - Adamu na Hawa:

*Madhara Ya Dhambi Katika Maisha Ya Ndoa*

*Soma Mwanzo 3.7-19*

Bwana aliumba Bustani ya Edeni, akamuweka Adamu, mtu wa kwanza, na akampa jukumu la kuilima aridhi. Adamu aliishi paradiso nzuri. Uzuri wa uumbaji wa Mungu ulimzunguka. Ugonjwa, mateso na huzuni havikujulikana. Alifurahia Amani na utulivu. Hakuwa na maadui wala shaka. Angeweza kuishi milele na muumba wake hapoparadiso. Mtu angeweza kufikili katika hali hiyo, moyo wa Adamu ungejawa na furaha. Ndani ya moyo wake, hata hivyo, alijiisi utupu.

Mungu alilitambua hili na akasema: “si vyema huyu mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye. (Mwanzo 2:18). Richa ya Adamu kuishi na Mungu vizuri kwenye busitani ya paradiso, Mungu alimuumba ili atafute furaha ya kweli na kuishi na wenzake wa kufanan nae. Adamu hakuubwa kwaajili ya kuishi pekeake. Mwanzo 3 inatuambia kwamba Mungu aliwaumba wanyama na kuwaleta kwa binadamu ili awapatie majina. Ingawa “hakuonekana wa kumsaidia (Mwanzo 2:20b). Kulikuwa hakuna shaka kuwa Adamu aliwafurahia wanyama hawa. Walimfariji na walikuwa zawadi nzuri kutoka kwa Mungu. Tatizo lilikuwa, hawakuweza kuuzipa utupu alio upata ndani ya Moyo wake. Wanyama hawa walimfanya Adamu aelewe Zaidi upweke wake.

Kukidhi hitaji hili kubwa, Mungu nalimfanya Adamu alale. Alipo lala, Mungu alichukua moja ya mbavu zake na kutoka kwenye mbavu alimtenmgeneza mwanamke. Adamu nalipo mwona, alitambua kuwa alikuwa msaidizi ambaye moyo wake ulimtaka. Alikuwa sehemu yake. Aliumbwa kutoka katika mwili wake. Adamu

alitambua muunganisho huo. Na alimuita “mwanamke” kwasababu alisema, “sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa ‘mwanamke’ kwamaana ametwaliwa katika mwanaume” (Mwanza 2:23). Waliubwa kwaajili ya kila mmoja wao. Walijitosheleza.

Tunaweza kufikili ni kwa jinsi gani kwa miezi michache ya mwanzo walivyo kuwa kama Adamu na Hawa walivyo ishi kwenye paradiso mbila na dhambi wala mateso. Hakuna kilicho watenganisha. Walifurahia ukamilifu na usawa wa mahusiano yao. Hakuna kilichokuwa kizuri Zaidi.

Mahusiano haya mazuri hayakudumu, hata hivyo. Mwanza 3 tunasoma historia ya jinsi ngani shetani alimjalibu Hawa kula kwenye mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Kushindwa kwa jaribu hili, alikula tunda lililo katazwa na kumpa mme wake. Kwa pamoja walikiuka moja kwa moja amri ya Mungu ya kutokula tunda la mti huu. Kupitia kwako, dhambi ikaingia kwenye bustani, dhambi hii ingeleta athari kubwa katika uhusiano wao kama wanandoa.

Mwanzo 3:7, tunasoma kwamba Adamu na Hawa walitambua kuwa walikuwa uchi na haliona aibu. Kwa mara ya kwanza kwenye maisha yao. Walijiisi kuwa wanakitu cha kuficha kwa kila mmoja. Hawakuweza tena kuwa na uhuru na ukaribu walio kuwa nao. Kwa matokeo ya aibuhii, Adamu na Hawa walirudi nyuma, na kutengeneza mipaka katika mahusiano yao.

Mwanzo 3:11-13 Mungu alikuja kwenye bustani kumuona Adamu na Hawa. Walipogundua kuwa Mungu alikuwa katikati yao, walijificha. Mungu alipo wauliza kwanini wanajificha, majibu ya Adamu yalionyesha dhahili. Alimwambia Mungu kuwa Hawa alimpa tunda kutoka kwenye mti ulio katazwa na akalila. Hakuna mhusika aliye tayari kukubali sehemu yake katika dhambi. Wanalaumu matendo yao kwa gharama ya mwingine.

Unaona kinachotokea hapa? Kiburi kimeingia kwenye maisha yao. Walikuwa teyari kuumfanya mwingine aonekane mbaya ili kujitetea. Kwa kuingia kwa dhambi kwenye Dunia. Adamu na Hawa waliona mabadiliko makubwa kwenye maisha yao ya ndoa yao. Walianza

kufikilia juu yao mwenyewe. Waliweza kusingizia matendo yao kwa gharama ya mwenza wake.

Haya hayakuwa madhara pekee ya dhambi katika maisha ya ndoa yao. Kama wanandoa, walipata maumivu na mateso kwa mala ya kwanza. Adama alihitajika kufanaya kazi kwa bidii ili kuilisha familia yake. Hawa atapata watoto kwa maumivu makali. Watapata maumivu sio tu ya kimwili lakini pia maumivu ya hisia. Walipata maumivu ya mauwaji ya kwanza kupitia mtoto wao Kaini kumuua ndungu yake kwa hasira za wivu. Watoto wao walikuwa chini ya dhambi kwenye maisha yao. Waliwapa wazazi wao wasiwasi. Kwa kufurahiya furaha ya paradiso, basi ilikuwa kidonge kichungu sana kwa Adamu na Hawa kumeza.

Uzuri na umoja wa mahusiano ambao Mungu aliuumba uliharibiwa na dhambi. Kila ndoa baada ya Adamu na Hawa lazima iishi na madhara ya dhambi na kwenye maisha ya ndoa.kwasababu ya dhambi, tunapambana na kiburi na ubinafsi. Tumekuwa na migogoro ambayotungeweza kuiepuka tu pale tunapoacha kujifikilia sisi wenyewe na kuanza kuwafikilia mwenzetu. Ni matatizo mangapi kwenye ndoa ambayo chanzo chake ni dhambi? Adui mkubwa kwenye ndoa ni dhambi.

Kwasababu ya dhambi, wanaume na wanawake lazima wafanye kazi kwa bidii katika dunia hii iliyo laaniwa nadhambi ili wameze kupata mahitaji yao muhimu kwa familia zao. Watoto wetu wanazaliwa na asili ya uovu. Lazima tupambane kuwaweka katika njia iliyo sahihi, hatakama tunajikuta tunadondokea kwenye dhambi hiyohiyo. Tumekosa usingizi mara ngapi kwaajili ya watoto wetu na tabia zao za dhambi?

Dhambi imekuwa na athari kubwa katika maisha yetu kama wanandoa kama unataka kuwa na mahusianao mazuri na mwenza wako, lazima upambane na dhambiu. Yesu pekee anaweza kukupa ushindi dhidi ya dhambi. Tatizo lilianza kwa Adamu na Hawa pale walipo mwacha Mungu. Kitu pekee amabacho unaweza fanya juu ya ndoa yako ni kuwa na uhakika kuwa unatembea na Mungu na unatafuta msamaha wake na kumruhusu apambanae na tabia yako ya dhambi. Ni pale tu ambapo mahusiano yako na Mungu yapo

sawa basina mahusianmo yako na mwenza wakoyatakuwa sawa. Jiweke kwenye mahusiano mazuri na Mungu na mahusiano yako na mwenza wako yatakuwa sawa.

Adamu na Hawa waliharibu mahusiano yao kwa sababu walimkiuka Mungu na kusikiliza sauti zao za dhambi. Dhambi hiyo iliharibu ndoa yao. Wakati mwigine unapokuwa natatizo kwenye ndoa yako, jiulize mwenyewe: ni dhambi gani amabyo inatuzuia sisi tusifurahie mahusiano ambayo Mungu alipanga tufurahiye? Utakapo pata majibu ya swali hilo, tubu dhambi na urudishe mahusiano mazuri na Mungu pamoja na mwenza wako.

Yakuzingatia:

Fikilia mara ya mwisho wewe na mwenza wako mmlikuwa na ugomvi. Ni kwa namna gani ugomvi huu ungeepukika kama usingejijari wewe sana na kumjali mwenza wako sana? Ulikuwa na hatia ya dhambi katika hali hii?

Adamu na Hawa waliona aibu kwa sababu ya dhambi zao. Walijaribu kuificha aibu hiyo kutoka kwa kila mmoja. Njinsi gani kuungama dhambi kwa wenzetu kunaweza kusaidia kwenye ndoa zetu. Utafanya nini kwa vitendo ambacho kitawasaidia watoto wako kuishinda dhambi kwenye maisha yao.

Kwa Maombi:

Muombe Mungu akusaidie kupambana na dhambi ya majivuno kwenye ndoa yako. Muombe akufungue macho kwa jinsi anavyoweza kumuhudumua mwenza wako na watoto wako.

# 2 - Ibrahimu na Sara:
*Swali La Kutii*

*Soma Mwanzo 12:10-15; 1 Petro 3:1-6*

Nabii Petro,aliwaandikia wanawake, akawaamuru wawatii waume zao ili wengine wavutwe kwa mwenendo wao mzuri.(1 Petro 3:1). Aliwatia moyo kumuangalia Sara mke wa Ibrahimu , kama mfano wao:

"*Maana hivyo ndivyo walivyojipamba wanawake watakatifu wa zamani waliomtumaini Mungu,na kuwatii wanaume zao, kama vile Sara alivyo mtii Ibrahimu, akamwita Bwana; nanyi ni watoto wakwe mfganyapo mema, wala hamkutishwa kwa hofu yoyote"(1Petro 3:5,6)*

Tunajua nini kuhusu Sarah kumtii Ibrahimu? Mwanzo 12 inatuambia historia ya Ibrahimu na Sara kwenda Misri kwasababu ya njaa kubwa katika aridhi ya Kaanani. Walipokuwa wanasafiri, Ibrahimu kwa kuogopa wanamisiri, kumuona mke wake mzuri, wangemuuwa na kumchukua mke wake. Ingawa alijua kuwa, wangewatendeavyema yeye na mke wake Sara kama wangejua kuwa alikuwa dada yake. Akamuomba Sara, ili aseme kuwa alikuwa dada yake. Huu haukuwa uongo moja kwa moja, tukisoma Mwanzo 20.12 kuwa Ibrahimu na Sara walikuwa na baba, mmoja lakini mama tofauti. Ingesemwa kuwa ndoa hii, wakati wa Musa ingekuwa sio ndoa harali.

"*Utupu wa umbu lako, binti ya baba yako, au binti ya mama yako, kwamba alizaliwa nyumbani mwenu au kwamba alizaliwa kwengine utupu wa hao usifunue"( Mambo ya walawi 18.9).*

Ibrahimu alitaka kutumua ukweli kuwa sara ni dada yake kwa manufaa. Kipindi hakusema uongo juu ya Sara kuwa dada yake,

alikuwa anaficha ukweli: kuwa alikuwa mke wake pia. Kwa sababu ya ukweli wa juu juu, Sara alipelekwa kwenye nyumba ya Farao na akajiweka kwenye hatari ya uzinzi ili kumuokoa mme wake.

Hii haikuwa mala ya mwisho kwa Sara kusimama kwaajili ya Mume wake. Badae katika Mwanzo 20 na Sara akamwambia mfalme Abimeleki uongo huohuo. Abimeleki alimchukua Sara kwenye nyumba yake na yeye. Kwa furaha, Bwana anamrinda Sara na uadilifu wake kwa kutomruhusu mfalme kukutana nae kimwili (ona mwanzo 20:6).

Kwenye matukio haya, Sara alitii kwa mme wake, Ibrahimu. Kwa upande mwingine, tunaweza mweshimu mke ambaye alikuwa teyari kumrinda mme wake. Alijitoa kwaajili yake. Usalama wa mme wake ulikuwa wasiwasi wake mkubwa. Alijitoa sana kwa hili. Nafikilia, hata hivyo, hili halikuwa rahisi kwa Sara. Siamini kuwa alitaka asiwe mwaminifukwenye tendo la ndoa kwa Ibrahimu. Nadhani pale mfalme alipomchukua aliomba kwa Mungu wake ulinzi. Hakutaka kumpoteza Mme wake. Hakuwa na furaha ya siku kuficha siri hii. Alitii. Hata hivyo, njee ya heshima kwa Ibrahimu na usalama wake aliaminishwa kuwa angeweza kupoteza maisha kama angeshindwa kutunza siri yao ya ndoa. Tutaludi tena kwenye stori hii badae kidogo.

Mwanzo kumi na sita, tunasoma kuwa Ibrahim, nae pia, alimtii mke wake Sara. Sara hakupata mototo. Akaamua, kumpa Ibrahimu msaidizi wake ili kwamba atapata mototo kupitia yeye. Kutokana na utamaduni wa siku hizo, kwasababu mfanya kazi alimilikiwa na Sara, basi mototo atakae zaliwa atakuwa mototo wa Sara. Ibrahimu alikubali ombi hilo na kulala na mfanyakazi wa Sara hajiri. Hajiri alipo gundua kuwa anamimba na atamzalia Ibrahimu mototo, alianza kumzalau Sara. Wivu mkubwa ulijitengeneza kati ya wanawake wao. Kwa mda, Sara alimlaumu Ibrahimu kwa matatizo yake na Hajiri:

*“Ubaya ulionipata na uwe juu yako; nimekupa mjakazi wangu kifuani kwako, naye alipoona kwamba amepata mimbaq, mimi nimekuwa duni machoni pake. Bwana na ahukumu kati ya mimi na wewe.”(Mwanzo 16.5)*

Labda kwa kuthibitisha upendo wake kwa Sara, Ibrahimu alimpa ruhusa mke wake kufanya kitu chochote akitakacho kwa mfanya kazi wake. Sara alimtendea vibaya kiasi cha Hajiri kukimbia.

Matukio haya mawili kwenye maisha ya Ibrahimu na Sara yanatuacha tunachanganyikiwa. Ni kwakiasi gani natakiwa kutii kwa mme au mke? Je, Sara alifanya vyema kutii kwa mume wake ingawa kutii huko kungemfanya yeye aanguke kwenye dhambi ya uzinzi? Je, Ibrahimu alifanya vyema kumtii mke wake na kumruhusu afanye chochote alichotaka na kumfanyia vibaya binadamu mwenzake? Kujibu maswali haya, tunatakiwa kuangalia kwa mtume Paulo.

Waefeso 5: 22, tunasoma:

*Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wenu (waefeso 5:22)*

Mafundisho ya Paulo katika hatua hii ni wazi. Mke anapaswa kunyenyekea kwa mume. Kwa kufanya hivyo, yeye ni mtiifu kwa Bwana. Swali, hata hivyo, linabaki: Je, anapaswa kujinyenyekeza kwa mume wake ikiwa hii inamaanisha kutomtii Bwana?

Kile ambacho Paulo aliwaambia Waefeso katika Waefeso 5:22 haimaanishi kwamba wanawake wanapaswa kutii kila tamaa ya waume zao. Wanapaswa kujitiisha kwa waume zao kama vile wangemtii Bwana. Kwa maneno mengine, wakati utii wao kwa waume zao unaenda kinyume na kusudi la Bwana, hawatakiwi kunyenyekea. Wanapaswa kujitiisha kwa waume zao kwa njia ambayo kwa kufanya hivyo, wanajisalimisha pia kwa wenza na kusudi la Bwana kwa maisha yao.

Petro, alipokuwa akizungumza na Sanhedrin katika Matendo 5, anasema:

*“ ime`tupasa kumtii Mungu  kuliko wanadamu.” (Matendo 5:29 )*

Huu ni mstari muhimu katika muktadha wa ndoa pia. Mke anapaswa kuwa mtiifu kwa mumewe lakini pia atambue kwamba ana mamlaka ya juu ambayo ni lazima anyenyekee. Ikiwa kwa

kujisalimisha kwa mumewe, mke anaasi amri ya Mungu, anajifanya kuwa na hatia mbele za Mungu. Kwa hiyo, mke anapaswa kujitiisha kwa mume wake kwa kuwa hilo halimfanyi kuyaacha mapenzi makubwa zaidi ya Mungu.

Je, Sara alifanya vyema kutii mapenzi ya Abrahamu alipomwomba afiche uhakika wa kwamba walikuwa wamefunga ndoa? Ninaogopa kwamba ikiwa kwa kufanya hivyo, angeasi amri kuu ya Mungu, alikuwa na hatia kweli. Nakuacha uamue mwenyewe. Hata hivyo, tunachohitaji kuchukua kutokana na mfano huo ni uhakika wa kwamba Sara alikuwa tayari kuweka kando mapendezi na tamaa zake kwa ajili ya mume wake. Hakuogopa kuteseka kwa ajili ya Ibrahimu. Alimwona kuwa muhimu zaidi kuliko yeye mwenyewe. Alikuwa tayari kufa mwenyewe kwa ajili ya mume wake. Ni mtazamo huu unaosifiwa na Sara. Je, ni matatizo mangapi yangeweza kuepukwa katika ndoa ikiwa wake wangekuwa na mtazamo kama huo? Kwa kweli, ni mtazamo wa Kristo kwetu. Alikuwa tayari kufa ili mimi na wewe tuishi. Mtazamo wa aina hii unahitaji kuweka maslahi ya mwenzi wako juu ya yako. Paulo aliiweka hivi:

*"lakini kama vile kanisas limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo." (Waefeso 5:24)*

Je, kanisa linapaswa kujinyenyekeza kwa Kristo jinsi gani? Anahitaji kufa mwenyewe na kumpa nafasi ya kwanza katika maisha yake. Anahitaji kuwa tayari kumtumikia na hata kuwa tayari kufa kwa ajili yake. Je, hii ni sifa ya uhusiano wako na mumeo?

Hatupaswi kuishia hapa. Katika Waefeso 5, Paulo pia ana baadhi ya maneno ya kumwambia mume. Sikiliza kile Paulo anachowaambia:

“*enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neon, apate kujiletea kanisa tukufu,lisilo na ila walakunyanzi wala lo lote kama haya; bali liwe takatifu , lisilo na mawaa. Hvivyo hivyo imewapasa waume nao*

*kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendae mkewe hujipenda mwenyewe." ( Waefeso 5:25-28 )*

Paulo aliweka wazi kwamba mume anapaswa kumpenda mke wake kama Kristo alivyolipenda kanisa. Kristo alipendaje kanisa? Ingawa Yeye ni Bwana, hakujifikiria Mwenyewe. Kila kitu alichofanya kilikuwa kwa ajili yake. Alijinyenyekeza na kufa kwa ajili yake. Paulo anatuambia kwamba Kristo alifanya hivyo ili kumtoa bibi-arusi Wake kwa Mungu kama bibi-arusi asiye na "waa wala kunyanzi."

Hebu turudi kwenye mfano wa Ibrahimu kwa muda mfupi. Je, Ibrahimu alikuwa akitafuta kumpeleka mke wake mbele za Mungu bila doa wala kunyanzi alipomwomba afiche ndoa yao? Je, alihangaikia kumtoa mke wake kwa Bwana bila lawama na bila dosari alipompa ruhusa ya kumtesa mtumishi wake? Inawezekana kabisa kwamba Ibrahimu hakuwa akifikiria kuhusu mambo ya kiroho hapa. Wasiwasi wake pekee unaonekana kuwa kujilinda na kujisaidia kutokana na mapigano ya mara kwa mara kati ya mke wake na mtumishi wake.

Ikiwa waume watakuwa viongozi wa familia ambao Kristo alikusudia wawe, lazima wanyenyekee kama vile Kristo alivyojinyenyekeza kwa ajili yetu. Ni lazima wawe tayari kufa kwa maslahi yao ili kutafuta maslahi ya wake na watoto wao. Kama viongozi wa nyumbani, lazima waongoze familia zao katika ufahamu mkubwa zaidi wa Kristo na makusudi yake kwao. Ili kufanya hivyo, lazima waishi na kuongoza kama watumishi. Hatimaye, ndoa ambayo Mungu anakusudia tuwe nayo ni ile ambayo pande zote mbili hutafuta mema ya mwingine. Ingawa Mungu amemwita mume awe kichwa cha familia, daraka hilo lazima litekelezwe kwa roho ya ujitiisho. Fikiria ufafanuzi ufuatao wa uwasilishaji na mamlaka:

***Utii***

*Kutii hakumaanishi kutendewa kama mtumwa*

*LAKINI*

*Kutii kunamaanisha kuweka masilahi yake juu yangu*

*Kutii haimaanishi kamwe kushukuru*

*LAKINI*

*Kutii kunamaanisha kuvumilia hata kama hakuna shukrani*

*Kutii haimaanishi kutoruhusu maoni yangu kamwe yajulikane*

*LAKINI*

*Kutii kunamaanisha kumruhusu atoe maoni yake*

*Kutii hakumaanishi kila wakati kusema “ndiyo” hata inapopingana na mamlaka kuu ya Mungu*

*LAKINI*

*Kutii kunamaanisha kufuata kielelezo cha Bwana wangu Yesu ambaye, akijiacha, alifikia hatua ya kufa kwa ajili yangu.*

***Mamlaka***

*Mamlaka haimaanishi kumdhulumu mke wangu*

*LAKINI*

*Mamlaka inamaanisha jukumu la ziada la kutunza na kuheshimu mtu wake*

*Mamlaka haimaanishi kuwa na mke wa kukidhi mahitaji yangu yote*

*LAKINI*

*Mamlaka inamaanisha kuwajibika kwa Mungu kwa mahitaji yake*

*Mamlaka haimaanishi kushinda kila hoja*

*LAKINI*

*Mamlaka haina maana ya kutafuta suluhu kwa kutoelewana kwetu kwa kutilia maanani maslahi yake*

*Mamlaka haimaanishi kumweka mahali pake*

*LAKINI*

*Mamlaka inamaanisha kufuata mfano wa Bwana wangu Yesu ambaye alienda kama Bwana na Mwalimu msalabani kwa ajili ya bibi arusi wake, Kanisa*

Kuzingatia:

Wake wanafikiria mfano wa ujitiisho wa Sara kwa Ibrahimu. Mfano wake unakusaidiaje kuelewa vizuri zaidi kile ambacho Mungu anatazamia kutoka kwako katika uhusiano wako na mume wako? Fikiria mfano wa vitendo katika ndoa yako ambapo unaweza kuweka kanuni hii katika vitendo.

Waume, mnajifunza nini katika sura hii kuhusu wajibu wenu wa kiroho katika familia? Maamuzi unayofanya katika familia yako yana lengo lao la kumleta mke na watoto wako mbele za Mungu bila "waa wala kunyanzi" kadiri gani. Unapaswa kufanya nini ili kuboresha?Je, inaweza kusemwa kwamba mamlaka ya mume juu ya mke katika Maandiko ni aina ya utii? Fikiria mfano wa Kristo. Unajifunza nini kutokana na mfano Wake?

Chukua muda wiki hii kufikiria jinsi unavyoweza kumhudumia mwenzako. Jiulize swali: ninawezaje kufa kwa nafsi yangu na kumsaidia wiki hii?

Kwa Maombi:

Mume:

Mwombe Bwana akusaidie kuwa kiongozi aliokusudia uwe. Mwombe akusaidie kuongoza kwa kuwa mtumishi wa mke wako, kama Kristo alivyolifanyia kanisa.

Mke:

Mwombe Bwana akusaidie kutanguliza masilahi ya mume wako kabla ya yako mwenyewe kama vile Kristo alivyowafanyia watu wake.

# 3 - Lutu na Mkewe:

*Nira Isiyo Na Usawa*

Soma Mwanzo 19:12-26

Lutu alikuwa mwana wa Harani ndugu wa Ibrahimu. Harani alikufa wakati Ibrahimu alipokuwa akiishi katika nchi ya Uru. Harani alipokufa, Ibrahimu alimchukua Lutu katika safari yake ya kwenda nchi ya Kanaani. Hatuelezwi Lutu alikuwa na umri gani baba yake alipokufa, lakini ni wazi kwamba hakuwa na umri wa kutosha kuwa peke yake. Ibrahimu alimlea Lutu kama mwana wake mwenyewe.

Katika Mwanzo 13, tunasoma kwamba Ibrahimu alisafiri hadi nchi ya Misri kwa sababu ya njaa kali iliyoharibu mashambani. Aliporudi kutoka Misri, wachungaji wake na wachungaji wa Lutu walianza kugombana kwa sababu hapakuwa na nafasi ya kutosha katika nchi ya kukaa pamoja. Tunaona kutokana na hili kwamba Lutu alikuwa kijana aliyewajibika kwa mifugo yake. Ibrahimu aliamua kwamba wakati ulikuwa umefika kwa Lutu kuwa peke yake. Ibrahimu alimpa chaguo la nchi kumiliki. Lutu alichagua uwanda wa Yordani kwa sababu ya udongo wake wenye rutuba na kumwacha Ibrahimu aanze maisha yake mapya. Kufikia hapa, hatujataja Lutu kuwa na mke.

Alipofika katika uwanda wa Yordani, lutu aliamua kuishi katika jiji la Sodoma. Mji huu ulikuwa mji mwovu, na wenyeji wake walikuwa wenye dhambi mbele za Bwana (Mwanzo 13:13). Uamuzi wa kuishi katika jiji hili ungekuwa mbaya. Wakati ujao tunaposoma kuhusu Lutu, yeye ni mwanamume aliyeoa na mwenye familia. Lutu alipata wapi mke wake? Je, inawezekana kwamba alioa mmoja wa wanawake wa kipagani wa jiji la Sodoma?

Ingawa Lutu alijua kuhusu Mungu wa Ibrahimu na alikuwa amekulia kwa muda katika familia ya mtakatifu huyu mkuu wa Mungu,

aliikataa imani ya Ibrahimu. Alioa mke asiyeamini na akachagua kuishi katika jiji lenye uovu.

Siku moja baadhi ya malaika kutoka kwa Mungu walifika katika mji wa Sodoma. Walikuja na neno kutoka kwa Bwana kwa Lutu. Mungu alikuwa anaenda kuharibu Sodoma na wakazi wake kwa sababu ya dhambi zao. Ingawa Lutu alikuwa hatembei tena na Bwana, alikuwa na usikivu wa kutosha kwa sauti Yake hivi kwamba aliuchukulia ujumbe huu kwa uzito. Labda alijua ndani kabisa ya moyo wake kwamba Mungu wa Ibrahimu ndiye Mungu wa kweli. Akiwa ameamini yale ambayo malaika walikuwa wamemwambia, aliionya familia yake juu ya hatari iliyokuwa inakuja. Pia alizungumza na wakwe zake wa baadaye kuhusu tangazo la malaika. Familia yake ilikataa kusikiliza. Waliamini alikuwa anatania. Hawangemchukulia kwa uzito.

“*lutu akatokaakasema na wakweze, waliowaposa bint zake, akasema, ondokeni mtoke katika mahali hapa kwa sababu Bwana atauharibu mji huu. Lakin akawa kama achezaye machoni pa wakweze.” ( mwanzo 19.14 )*

Lutu hakujua la kufanya. Malaika walimtia moyo aondoke jijini mara moja, lakini akasitasita. Hakutaka kuiacha familia yake nyuma. Malaika walipoona kwamba haondoki, wakamshika mkono, mkewe na binti zao wawili, wakawatoa nje ya mji. Wakiwa nje ya jiji, malaika waliwaonya wakimbie na wasiangalie nyuma. Hawakupaswa kusimama hata kwa mara moja, kwa sababu hukumu ya Mungu ilikuwa karibu kuuangukia mji huo (Mwanzo 19:17).

Licha ya onyo la malaika, Biblia hutuambia kwamba mke wa Lutu alitazama nyuma. Sidhani kama hiki kilikuwa kitendo rahisi cha udadisi. Ninaamini kwamba alikuwa anashangaa kwa nini alikuwa akiondoka mjini. Hakutaka kuondoka. Maisha yake yalikuwa Sodoma. Moyo wake ulikuwa pale pia. Alipenda njia za Sodoma. Hakuwa tayari kutoa vitu hivi. Kwa sababu ya moyo wake wa kutokuamini na kutotii, Bwana alimpiga peke yake pamoja na wakazi wengine wa Sodoma.

Kwa habari ya binti wawili wa Lutu, walipoona kwamba wamefiwa na mama yao na waume wao wa baadaye, waliamua kumlewesha Lutu kwa divai na kulala na baba yao ili kuendeleza nasaba yao. Kwa uvutano wa divai, Lutu alilala na binti zake, ambao walipata mimba na kuzaa wana wawili.

Petro anatuambia jambo la kupendeza kuhusu Lutu:

*"akamwokoa Lutu, yule mwenye haki aliyehuzunishwa sana na mwenendo wa ufisadi wa hao wahalifu(kwa maana mtu huyu akikaa kati yao, kwa kuona na kusikia, alijitena roho yake yenye haki, siku baada ya siku, kwa matendo yao yasiyo na sheria). ( 2 Petro 2:7, 8)*

Kulingana na Petro, Lutu alikuwa mtu mwadilifu ambaye aliteswa mfululizo katika maisha yake kwa sababu ya dhambi. Aliteswa siku baada ya siku kwa sababu ya maovu aliyoyaona huko Sodoma. Ingawa alimpenda Mungu, alinaswa katika mtego. Alikuwa ameoa mke ambaye hakumpenda Bwana. Aliishi katika mji wa upotovu. Alikuwa akiwapoteza watoto wake kwa mivuto ya jiji hili lenye dhambi ambalo alikuwa amechagua kuishi. Mambo hayo yote yalimlemea Lutu. Walimtesa kila siku. Hakuwa na amani na nafsi yake wala na Mungu wake.

Kwa sababu mke wake hakumpenda Bwana, Lutu hakuweza kusema mengi wakati binti zake walitaka kuolewa na wanaume ambao hawakumjua Bwana. Kwa sababu fulani, alitoa idhini yake kwa ndoa hizi. Akiwa kiongozi wa kiroho wa familia yake, Lutu alishindwa kuongoza familia yake katika ujuzi na upendo wa Mungu. Haya yote yalianzia wapi? Kila kitu kilianza alipochagua kuishi katika mji mwovu wa Sodoma na kuoa mke ambaye hakumpenda Bwana. Lutu, ambaye alikuwa dhaifu katika imani yake, kwa kuchagua kuoa mke asiyeamini, alitangatanga kutoka kwa Bwana. Mke wake hakumtia moyo atembee katika njia za Yehova. Ikiwa kuna chochote, aliumiza mwendo wake wa kiroho. Hata watoto wake walivutwa katika ushawishi mbaya wa mazingira yao. Lutu alipoamua kuongea nao juu ya mambo ya Mungu, walikataa kusikiliza. Alikuwa amepoteza sifa zote kama kiongozi wa kiroho katika familia yake.

Je, nini kingetokea kama Lutu angechagua mke ambaye alimpenda Bwana kikweli? Je, hilo lingeleta tofauti gani katika maisha yake na ya watoto wake? Ingawa hii inaweza kuwa uvumi mtupu, nina maoni kwamba maisha yake yangekuwa tofauti sana. Badala yake, sasa aliishi maisha ya mateso kwa sababu alijua alikuwa ameshindwa katika kutembea kwake na Bwana. Alijua pia alikuwa na jukumu la kupoteza mke na binti zake kwa dhambi ya Sodoma?

Biblia inatuonya kuhusu hatari za kuoa au kuolewa na mtu asiye mwamini. Kutoka 34:15,16 inatuambia:

“*usije ukafanya agano na wenyeji wan chi, watu wakaenda kufanya uzinzi na miungu yao na kuitolea sadaka miungu yao;mtu mmoja akakuita,ukaila sadaka yake ukawaoza wana wako binti nzao, nao binti zao wakaenda kufanya uzinzi na miungu yao,wakawavuta wana wenu wafanye uzinzi na miungu yao .” (Kutoka 34.15,16)*

Katika Kumbukumbu la Torati 7:3, 4, tunasoma:

*“binti yakko usimpe mwanawe mume, wala usimtwalie mwanao mume binti yake, kwa kuwa atamkengeusha wanao mume aszinifuate, ila wapate kuabudu miungu mingine; ndipo itakapo waka hasira ya Bwana juu yenu, naye atakuangamiza upesi.” ( Kumbukumbu la Torati 7:3, 4 )*

Hiki ndicho hasa kilichotokea katika maisha ya Lutu. Maisha yake yaliokolewa kwa sababu tu ya maombi ya mjomba wake Ibrahimu kwa Mungu kwa niaba yake.

Agano Jipya pia liko wazi kabisa:

“*Msifungwe nira pamoja na wasioamini. kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uaswi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza. Tena pana ulinganifu ngani kati ya Kristo na Beliari? Au yeye asiyeamini?” ( 2 Wakorintho 6:14, 15 )*

Mwanamume au mwanamke anayefikiria kuoa au kuolewa na asiyeamini anapaswa kuzingatia onyo la neno la Mungu. Wana

hatari ya kutangatanga kutoka kwa Mungu. Wana hatari ya kupoteza watoto wao kwa dhambi na ulimwengu kutokana na mfano wao mbaya. Wana hatari ya kugawanya familia zao. Wana hatari ya kupoteza ushawishi wote kwa wema katika maisha ya familia yao kwa sababu ya maelewano yao. Biblia inatupa mfano wenye kuhuzunisha katika hadithi ya Lutu ya mume na mke waliokuwa wamefungwa nira isivyo sawa. Ikiwa haujafunga ndoa kwa sasa, jitolee leo kuoa mwenzi tu ambaye anampenda Bwana kweli na anatembea naye. Usifuate mfano mbaya wa Lutu.

Kuzingatia:

Je, una ushawishi wa aina gani wa kiroho katika maisha ya mwenzako? Je, ushawishi huu umekuwa kwa manufaa? Nini kifanyike ili kuboresha hali hii?

Je! unawapa watoto wako mfano gani wa kiroho? Nini kifanyike kuboresha hali hii.

Ikiwa hujaolewa, somo hili linakufundisha nini kuhusu umuhimu wa kuoa au kuolewa na mwamini ambaye amejitolea kutembea na Bwana? Ikiwa sasa umefunga ndoa na mtu asiye mwamini, unapata matatizo gani? Unaweza kumpa shauri gani kijana anayefikiria kufunga ndoa na mtu ambaye si mwamini?

Kwa Maombi:

Ombea mtu unayemfahamu ambaye ameoa mtu asiyeamini. Ombea pia wokovu wa mwenzi huyu asiyeamini.

# 4 - Isaka na Rebeka:

*Wanandoa Na Watoto Wao*

*Soma Mwanzo 27:1-10*

Ibrahimu sasa alikuwa mzee. Alikuwa na wasiwasi kwamba mwana wake Isaka atapata mke. Ilikuwa muhimu apate mke ili ahadi za Mungu za kumfanya kuwa taifa kubwa zitimie. Kwa sababu alikuwa mzee, Ibrahimu alimwita mtumishi wake na kumpa kazi ya kumtafutia mwanawe mke.

Sio tu mwanamke yeyote ambaye angemfanyia mwanawe Isaka. Kulingana na Mwanzo 24, Ibrahimu alikuwa na mahitaji mawili. Kwanza, ilikuwa ni lazima kwamba mwanamke huyu awe kutoka kwa familia yake mwenyewe. Hakupaswa kuchaguliwa kutoka kwa mataifa ya wapagani wasioamini. Mungu alikuwa anaenda kutimiza makusudi yake kupitia wanandoa hawa. Ilikuwa muhimu kwamba familia yao iwe na msingi juu ya Mungu na Sheria yake.

Pili, ilikuwa lazima kwamba mwanamke huyo awe tayari kuondoka katika nchi yake na kuwa mke wa Isaka. Hakupaswa kulazimishwa katika ahadi hii. Alihitaji kuhisi moyoni mwake kwamba Bwana alikuwa akimsukuma kuolewa na Isaka.

Mtumishi wa Ibrahimu alikubali jukumu la kwenda katika misheni hii. Kulingana na Mwanzo 24:10, aliondoka kwenda Mesopotamia ambako familia ya Ibrahimu iliishi. Alipofika Mesopotamia, alikuta kisima ambacho alijua wanawake wa mji huo wangetoka kuteka maji. Pale kisimani, aliomba mwongozo wa Bwana. Huu ulikuwa uamuzi muhimu. Alihitaji uongozi na hekima ya Bwana.

Angalia jinsi Ibrahimu alivyoomba. Alimwomba Mungu ishara. Haikuwa tu ishara yoyote. Ishara hii ingemwonyesha mtumishi

tabia halisi ya mwanamke ambaye alikuwa akimtafuta Isaka. Alimwomba Bwana kwamba mwanamke ambaye angekuwa mke wa Isaka ampe yeye na ngamia wake kitu cha kunywa. Ingawa sijawahi kupata fursa ya kumpa ngamia mwenye kiu maji ya kunywa, naweza kufikiria kwamba hangekuwa jambo rahisi. Wanyama hawa wameundwa kuhifadhi maji kwa siku kadhaa za kusafiri kupitia jangwa la joto. Mwanamke aliyejitolea kumnywesha mtumishi na ngamia wake alikuwa ni mwanamke asiyejifikiria yeye tu. Alipendezwa na mahitaji ya wengine. Pia alikuwa mwanamke wa huruma. Hakuogopa kutumia bidii yake kwa mgeni kabisa na wanyama wake. Alikuwa mchapakazi. Alikuwa mkarimu. Je, ni kwa ajili ya sifa hizi kwamba mtumishi alikuwa anatafuta? Rebeka alipokuja kisimani, alithibitisha kuwa yeye ndiye aliyetajwa hapo juu.

Mtumishi wa Ibrahimu alijua mapenzi ya Mungu si tu kwa ishara aliyokuwa ameomba kutoka kwa Bwana, lakini pia alijaribu ishara hii. Kuna angalau thibitisho mingine mitatu wa mapenzi ya Mungu katika kifungu hiki. Ya kwanza ya uthibitisho huu ni uthibitisho wa familia yake. Mtumishi huyo alipomuuliza Rebeka kuhusu familia yake, aligundua kwamba alikuwa mtu wa ukoo wa Ibrahimu. Hii ilikuwa moja ya mahitaji ya bwana wake. Uthibitisho wa pili ulikuja kwa njia ya idhini ya mzazi ya ndoa. Mtumishi wa Ibrahimu aliwaambia jinsi Ibrahimu alivyomtuma na jinsi alivyosali kwenye kisima. Alieleza jinsi Rebeka alivyompa yeye na ngamia wake kitu cha kunywa, kama vile alivyoomba. Ushuhuda huu uliisadikisha familia ya Rebeka kwamba jambo hilo lilitoka kwa Bwana. Wakakubali ndoa.

Uthibitisho wa tatu ulikuja kwa njia ya ridhaa ya Rebeka. Ibrahimu alikuwa amemwambia mtumishi wake kwamba lazima mwanamke huyo awe mke wa Isaka kwa hiari. Familia ilipomwuliza Rebeka ikiwa alikuwa tayari kuacha nchi yake na familia yake ili kuolewa na Isaka, Rebeka alikubali. Yeye, pia, alihisi kwamba hayo yalikuwa mapenzi ya Mungu kwa maisha yake. Pamoja na uthibitisho huu wote, hakuwezi kuwa na shaka kwamba Rebeka alikuwa kweli mwanamke ambaye Mungu alikuwa amemchagua kuwa mke wa Isaka.

Biblia inatuambia kwamba Isaka alimpenda Rebeka (Mwanzo 24:67). Walikuwa na wana wawili walioitwa Yakobo na Esau. Walihangaikia hali njema ya kiroho ya familia yao wakiwa wenzi wa ndoa. Biblia inatuambia juu ya kukatishwa tamaa kwao wakati mwana wao Esau alipoamua kuoa mke asiyeamini (ona Mwanzo 26:34, 35).

Ndoa yao haikuwa kamilifu. Ni watoto wao ambao wangeweka kizuizi kati yao. Yote ilianza katika Mwanzo 25:27, 28:

*"Wavulana wakakua, Esau akawa mtu wa kuwinda wanyama hodari, mtu wa nyikani; Isaka, ambaye alikuwa akionja nyama pori, alimpenda Esau, lakini Rebeka alimpenda Yakobo."* *(Mwanzo 25:27,*28)

Upesi Isaka na Rebeka walianza kucheza na watoto wao. Rebeka daima alionekana kumlinda na kumpandisha Yakobo juu ya Esau. Siku moja, alimsikia Isaka aliyekuwa mzee akimwomba Esau mwana wake aende msituni na kumkamatia mnyama pori. Alikusudia kumpa Esau baraka zake kama mwana mkubwa. Akitaka kumpandisha cheo Yakobo juu ya Esau, Rebeka aliamua kumdanganya mumewe ili ampe baraka badala yake. Alimwambia mwanawe Yakobo amletee wanambuzi wawili. Aliwatayarisha na kumwomba aende kwa baba yake akijifanya kuwa Esau ili apate baraka za Esau. Ingawa Yakobo mwanzoni hakutaka kujihusisha na aina hii ya udanganyifu, mama yake alimsukuma, na hatimaye akakubali. Kwa pamoja wanafanikiwa kumdanganya Isaka.

Esau alipogundua kwamba baraka yake imeibiwa kutoka kwake, aliapa kwamba angemuua ndugu yake Yakobo. Aliposikia hivyo, Rebeka alimwambia Yakobo akimbilie familia yake huko Mesopotamia hadi hasira ya Esau ipungue. Ili kuhalalisha alichofanya, alienda kwa mume wake Isaka na kumwambia kwamba alikuwa na wasiwasi kwamba Yakobo angeoa mmoja wa wanawake Wakanaani wa eneo hilo. Alimtaka aende Mesopotamia kutafuta mke miongoni mwa watu wake. Hakuwa mwaminifu kwa Isaka. Alifanya hivyo ili kumlinda mtoto wake aliyempenda zaidi. Rebeka yuko tayari kumdanganya mumewe. Kwa kufanya hivyo, anaonyesha kutomheshimu katika uzee wake. Ni nini kilimsukuma

kufikia hatua hii? Je, haikuwa wivu wake kwa ajili ya hali njema ya mwana wake kipenzi Yakobo?

Je, tunajifunza nini kutokana na hadithi ya Isaka na Rebeka? Tunagundua jinsi wanandoa ambao walipendana na kuheshimiana kweli mwanzoni walivyotengana kwa sababu ya watoto wao. Ingawa watoto ni baraka halisi kutoka kwa Bwana, wanaweza pia kuja kati ya mume na mke.

Je, inawezekana kwamba una hatia, kama Isaka na Rebeka, ya kutoa upendeleo kwa mtoto mmoja kuliko mwingine? Je, unamwadhibu mtoto mmoja kwa ukali zaidi kuliko mwingine? Je, unatarajia zaidi kwa mmoja kuliko mwingine? Je, unatoa upendeleo maalum kwa mmoja juu ya mwingine? Hii inaweza kusababisha matatizo katika maisha ya familia yako. Inaweza hata kuleta mgawanyiko kati yako na mpenzi wako.

Je, umekuwa na mijadala mingapi mikali na mwenza wako kuhusu jinsi ya kulea watoto wako? Malezi ya watoto yanaweza kusababisha mgawanyiko mkubwa katika ndoa yako. Tunaweza kukazia fikira watoto wetu hivi kwamba hatusitawishi tena uhusiano wetu tukiwa wenzi wa ndoa. Wakati watoto hawa wanaondoka nyumbani kwetu, tunajikuta tunaishi na wenza ambao hatuwajui tena.

Wanandoa wowote wanatambua kwamba wakati una watoto, huna tena muda mwingi wa mpenzi wako. Mabadiliko ya vipaumbele. Watoto wetu sasa wanahodhi wakati tuliokuwa tukitumia katika mawasiliano na wenzi wetu. Kwa mara nyingine tena, hii inaweza kusababisha wanandoa kutengana.

Mtu fulani aliwahi kusema kwamba jambo bora zaidi ambalo mume anaweza kuwafanyia watoto wake ni kumpenda mama yao. Kuna ukweli katika kauli hii. Unaweza kuwa na uhusiano mzuri sana na watoto wako na ukakosekana katika maisha yako kama wanandoa. Hii inaweza tu kuwadhuru watoto wako. Katika siku zetu, watoto wanahitaji kuona mfano halisi wa mama na baba wanaopendana. Si rahisi kila wakati kupata uwiano kati ya wajibu wetu kwa wenzi wetu na watoto wetu. Jambo ambalo kutafakari huku

kunatufundisha, hata hivyo, ni kwamba tunapaswa kuwa waangalifu ili watoto wetu wasiweke kizuizi kati ya mume na mke. Mungu atusaidie tuwe na usawaziko unaofaa.

Kuzingatia:

Fikiria juu ya uhusiano wako na mwenzi wako. Je, uhusiano huu ni chanzo cha baraka kwa watoto wako? Je! watoto wako wanaona jinsi wewe na mwenzako mnapendana? Je, wana mfano kwako wa kufuata katika ndoa yao?

Je, kuna njia yoyote ambayo watoto wako wamekuchukua kutoka kwa mpenzi wako? Unaweza kufanya nini kubadilisha hili kwa manufaa ya watoto wako na mwenza wako?

Kwa Maombi:

Ikiwa una watoto, mwombe Bwana hekima katika kupata usawa kati ya uhusiano wako nao na mwenzi wako. Mwombe Hm akusaidie kama mume na mke kuwa kitu kimoja katika suala hili la kulea watoto wenu. Ikiwa kwa sasa huna watoto wowote nyumbani, waombee wanandoa wengine unaowajua. Mwombe Bwana hekima na usawa katika maisha yao.

# 5 - Yakobo na Lea:

*Mke Asiyependwa*

Soma Mwanzo 29:31-35

Kwa sababu ya udanganyifu wake, Yakobo alilazimika kuondoka katika nchi yake na kwenda Mesopotamia, ambako familia ya mama yake iliishi. Alikuwa amemdanganya kaka yake kutoka katika haki yake ya kuzaliwa na baraka. Sasa Esau akaapa kwamba atamwua Yakobo. Yakobo aliikimbia nchi yake ili kuokoa maisha yake.

Alipofika Mesopotamia, Yakobo alisimama karibu na kisima. Hapa ndipo wachungaji walipokusanyika ili kuwanywesha kondoo wao. Aliwauliza kama wanamfahamu Labani, ndugu ya mama yake. Walimjulisha kwamba mmoja wa binti za Labani alikuwa anakuja kisimani kunywesha kondoo wa baba yake. Ilikuwa kwa njia hii kwamba Yakobo alitambulishwa kwa Raheli.

Biblia inatuambia kwamba Yakobo alimpenda Raheli (Mwanzo 29:18). Alizungumza na baba yake kuhusu kumchukua kuwa mke wake. Labani alikubali kwa msingi kwamba Yakobo atamfanyia kazi miaka saba. Yakobo alikuwa tayari zaidi kufanya hivyo, na hivyo mapatano yakafanywa kati ya watu hao wawili. Hata hivyo, siku ya arusi yake, Labani alimpa Yakobo binti yake mkubwa Lea badala yake. Harusi ilikamilika, na udanganyifu haukugunduliwa hadi asubuhi iliyofuata. Yakobo hakuwa na furaha. Kwa hasira yake, Yakobo alikwenda kumwona Labani. Baba mkwe wake alimwambia kwamba haikuwa desturi kuoa binti mdogo kabla ya mkubwa. Alimuahidi binti yake mdogo Raheli ikiwa angemfanyia kazi miaka saba mingine. Jacob alilazimika kukubali.

Tunagundua kutoka kwenye Mwanzo 29:30 kwamba Yakobo alimpenda Raheli kuliko Lea. Hilo lilizua mvutano katika familia huku dada wote wawili wakipigania uangalifu wa mume wao. Lea angeteseka sana kwa miaka mingi katika vita hivi. Mungu aliona uchungu wake, hata hivyo, na akaja kumwokoa. Lea akamzalia Yakobo wana wengi. Raheli, hata hivyo, hakuweza kupata watoto.

Kinachovutia katika hadithi hii ni majina ya watoto wa Leah. Majina haya yanaonyesha mapambano makali aliyokuwa nayo katika vita vyake vya mapenzi ya mumewe. Mtoto wa kwanza wa Lea na Yakobo aliitwa Rubeni. Lea akampa jina hili kwa sababu alisema, “Ni kwa sababu Bwana ameona taabu yangu. Hakika mume wangu atanipenda sasa.” (Mwanzo 29.32b). Alitumaini kwamba kwa sababu alikuwa amempa Yakobo mwana huyu, angempenda.

Alipomzaa mwanawe wa pili, Lea akamwita Simeoni. Mwanzo 29:33 inatuambia kwamba alimpa jina Simeoni kwa sababu “Bwana alisikia ya kwamba sipendwi, akanipa huyu pia” (Mwanzo 29:33). Maumivu yake ni dhahiri. Anatafuta chochote ambacho kingemfanya Yakobo ampende. Anataka kupendwa.

Lea alimwita hapa mwana wa tatu, Lawi kwa sababu alisema, “Sasa, hatimaye, mume wangu ataambatana nami kwa sababu nimemzalia wana watatu (Mwanzo 29:34). Baada ya wana watatu na angalau miaka mitatu ya ndoa, Lea bado hajauvuta moyo wa mume wake. Bado anatamani kupendwa lakini anakosa usikivu wa mumewe.

Mwana wake wa nne alipozaliwa, Lea alimwita Yuda, linalomaanisha “sifa.” Ana hisi kwamba Bwana anambariki. Ingawa mume wake hakumpenda, Mungu hakuwa amemwacha. Kwa hili, angelisifu jina Lake. Baada ya hayo, Leah aliacha kupata watoto.

Raheli, ambaye Yakobo alivutiwa naye, aliona wivu moyoni mwake aliposhindwa kumpa mume wake mwana. Aliamua kumpa Yakobo mjakazi wake ili apate mtoto wa kiume kupitia kwake. Mwana huyu angekuwa mwana wa Raheli kwa sheria. Bilhadi akampa Yakobo mwana ambaye Raheli alimwita Dani kwa sababu alisema, “Mungu amenihesabia haki; amesikiliza ombi langu na kunipa mtoto wa

kiume (Mwanzo 30:6). Uthibitisho wake ulikuwa dhidi ya dada yake Lea ambaye alikuwa akimpa Yakobo wana wengi.

Bilha, mtumishi wa Raheli, alimpa Yakobo mwana wa pili. Raheli akamwita Naftali kwa sababu alisema, “Nimeshindana sana na dada yangu, nami nimeshinda (Mwanzo 30:8). Sasa alikuwa na imani fulani moyoni mwake kwamba usikivu wa Yakobo ulikuwa umegeuzwa vya kutosha kutoka kwa Lea tena.

Mapambano kati ya dada hawa wawili yaliendelea kwa miaka mingi. Alipoona vile Raheli amefanya, Lea pia alimpa Yakobo mtumishi wake na kupata wana wawili kupitia mtumishi wake Zilpa. Hatimaye Mungu alifungua tumbo la uzazi la Lea tena, naye akamzalia mumewe wana wengine wawili. Jina la mwanawe wa sita ni muhimu kwa utafiti huu. Anamwita Zebuloni kwa sababu alisema, “Mungu amenipa zawadi ya thamani. Wakati huu mume wangu ataniheshimu kwa sababu nimemzalia wana sita (Mwanzo 30:20).

Baada ya wana sita na zaidi ya miaka sita ya ndoa, Lea angali anapambana ili kupata utegemezo na upendo wa mume wake. Anataka mumewe ampende na kumheshimu. Ni hadithi ya kusikitisha iliyoje. Kwa miaka mingi Leah alikuwa ameolewa na mtakatifu huyu mkuu wa Mungu na hakuwahi kuwa na hakikisho la upendo wake. Inawezekana kwamba katika maisha yake yote ya ndoa, hakujua kama Yakobo alimpenda. Jambo la kusikitisha kuhusu hadithi hii ni kwamba ni kweli hata katika siku zetu. Je, ni waume na wake wangapi hawana uhakikisho wa upendo na kukubalika kwa wenzi wao?

Unafanya nini katika hali hii? Je, unaishughulikia vipi ndoa ambayo imeharibika? Tunaona mambo mawili katika maisha ya Lea ambayo yanapaswa kutusaidia kujibu swali hili. Kwanza, Leah hakuacha kujaribu kupata upendo na kibali cha mume wake. Mapambano haya yaliendelea kwa miaka. Ili kutatiza masuala, Lea alilazimika kushindana na mwanamke mwingine. Hili halikuwa rahisi kwake. Jaribio lingekuwa ni kuacha kujaribu na kuwa chungu na ngumu. Angeshawishika kumsukuma kando na kuyafanya maisha yake kuwa magumu. Angeweza kukata tamaa na kuendelea na maisha bila upendo wa mumewe. Alikataa kufanya

hivi, hata hivyo. Alikuwa amejiahidi kwa Yakobo, na angedumu katika uhusiano wake naye. Alijitolea kufanya kila awezalo ili ndoa yake ifanikiwe. Zaidi ya hayo, hata hivyo, alijitolea kupigania upendo wake. Hakutaka ndoa bila upendo. Upendo wake kwa Yakobo haukufa kamwe. Ingawa hakukamilishwa katika maisha yake mwenyewe, alijitolea kufanya kila awezalo kwa ajili ya mumewe. Ni mfano gani wa subira na upendo wa kweli tulionao katika hadithi ya Lea. Anatupa mfano mzuri wa kufuata.

Jambo la pili tunalohitaji kuona katika maisha ya Lea ni kwamba ingawa hakuwa na upendo na utegemezo wa mume wake sikuzote, alitiwa moyo na Mungu wake. Katika Mwanzo 29:32, alisema: “Bwana ameona taabu yangu (Mwanzo 29:32). Katika mstari unaofuata, anasema: “Bwana alisikia kwamba sikupendwa (Mwanzo 29:33). Alimsifu Bwana kwa ajili ya mtoto wake katika Mwanzo 29:35. Katika Mwanzo 30:20, alitambua kwamba mtoto wake alikuwa zawadi ya pekee kutoka kwa Bwana Mungu. Katika mambo haya yote, Lea alifahamu mkono wa Mungu ukifanya kazi maishani mwake. Alijua kwamba ingawa mume wake hakumpenda jinsi ambavyo angetaka, upendo na huruma ya Mungu kwake haikubadilika. Alipata faraja kubwa na uhakika katika hili. Inaweza kuwa hii ndiyo iliyomfanya aende kinyume na uwezekano wote.

Ni kweli kwamba uhusiano wa Lea pamoja na Mungu haukuondoa maumivu ya kukataliwa kwa mume wake, lakini ulimpa nguvu za kukabiliana na kukataliwa huko. Hata kama mume wake hakuwepo, Mungu hangemwacha kamwe. Je, uko katika hali ya Lea leo? Labda unahitaji kuhakikishiwa utunzaji na huruma ya Mungu. Kamwe hatakuacha wala hatakuacha. Ndani Yake, kuna nguvu na upendo wa kuendelea. Nguvu za Lea zilitoka kwenye uhusiano wake na Mungu.

Lea anatupa hapa mfano wenye nguvu sana wa kufuata. Ukiteseka kama Lea katika ndoa yako, Mungu na awe halisi kwako kama vile alivyokuwa kwake.

Kuzingatia:

Je, unaweza kujitambulisha na mapambano ya Leah? Unajifunza nini kutokana na mfano wake?

Mfano wa Kristo unatufundisha nini kuhusu jinsi ya kukabiliana na hali kama hizo?

Nguvu ya kustahimili hali kama Lea inatoka wapi? Ni nini kinazuia upokeaji wa nguvu hizi?

Labda una hatia ya dhambi ya Yakobo. Je, unahitaji kufanya nini ili kurekebisha mambo na mpenzi wako? Ni nini kinakuzuia?

Kwa Maombi:

Mwombe Bwana akusaidie kuonyesha upendo zaidi kwa mwenzako. Je, uko katika hali ya Leah kwa sasa? Mwombe Mungu awe halisi zaidi kwako. Je! unamjua mtu mwingine katika nafasi ya Leah? Wakabidhi wao na wenza wao kwa Bwana.

# 6 - Musa na Sipora:
*Uharibifu*

*Soma Kutoka 2:16-22*

Baada ya kulazimishwa kuondoka Misri, Musa alikimbilia nchi ya Midiani. Alisimama karibu na kisima ili kupumzika kutoka kwa safari yake. Alipokuwa akipumzika, wasichana saba walikuja kisimani wakiwa na kundi la kondoo. Walipokuwa wakinywesha mifugo yao, wachungaji fulani wabaya walikuja na kuwafukuza kondoo wao. Jambo hilo lilimkasirisha Musa, ambaye alichukua ulinzi wa wanawake hao, akawafukuza wachungaji hao waovu na kuwasaidia wanawake kurejesha kondoo wao. Hakujua kuwa kati ya wanawake hawa kulikuwa na mmoja ambaye angekuwa mke wake.

Musa alirudi na wanawake hao nyumbani kwao ambako alikutana na baba yao, mwanamume aliyeitwa Yethro. Muda si muda Yethro aligundua kwamba Musa hakuwa na mahali pa kwenda. Mwanamume katika nyumba yake angekuwa msaada kwa Yethro. Alimwomba Musa afikirie kukaa naye na kufanya kazi na kondoo wake. Tunaelewa kwamba, kwa Mmisri, kufuga kondoo ilikuwa kazi ya kuchukiza (ona Mwanzo 46:34). Wakati Musa alikuwa amekulia katika nyumba ya binti wa Farao, alilazimika kuweka historia yake kando na kujitengenezea maisha mapya. Alikubali ombi la Yethro na kukaa naye.

Sipora alikuwa mmoja wa binti saba wa Yethro. Akampa Musa awe mke wake. Sipora alimpa Musa mwana aliyeitwa Gershomu. Musa alichagua jina hili kwa sababu alisema, "Nimekuwa mgeni katika

nchi ya ugeni" (Kutoka 2:22). Walikuwa na mwana wa pili aliyeitwa Eliezeri kwa ukumbusho wa jinsi Bwana alivyomwokoa Musa kutoka kwa mkono wa Farao (Kutoka 18:4). Musa alitambua kwamba Midiani haikuwa nyumbani kwake. Alikuwa amekulia Misri, lakini alikuwa Mwisraeli aliyetengwa na watu wake. Alikuwa na mzigo mkubwa kwa watu wake na ukandamizaji wao katika nchi ya Misri. Wakati hili, Sipora hakuelewa jinsi hili lilivyokuwa zito mkubwa kwa Musa.

Miaka arobaini ilipita. Mungu alimtokea Musa katika kichaka kilichokuwa kinawaka moto. Alimwambia kwamba alitaka arudi Misri ili kuwakomboa watu wake kutoka katika utumwa wao. Hapo awali, Musa aliona vigumu kuamini kwamba Mungu angemwita kwa kazi hii. Hata hivyo, baada ya kushindana sana na Mungu, alikubali kazi hiyo. Mwanzo sura ya nne inatuambia kwamba Musa alifunga virago vyake, akamchukua mke wake na wanawe na kuanza safari ndefu ya kurudi Misri.

Wakiwa njiani kuelekea Misri, Bwana Mungu alimshambulia Musa na alitaka kumuua (ona Mwanzo 4:24). Tatizo lilikuwa nini? Tunapata jibu katika hatua ya Sipora. Akamchukua Gershomu, mwana wao, akamtahiri kwa kisu cha gumegume. Hapo ndipo hasira ya Mwenyezi-Mungu ikamtoka Musa. Tatizo inaonekana kuwa Musa hakuwa amechukua muda wa kumtahiri mwanawe. Zipora hakuwa Myahudi. Hakulelewa pamoja na watu wa Mungu. Lakini kama mgeni, yeye ndiye aliyemtahiri Gershomu kulingana na mapokeo ya Israeli. Sipora hakupendezwa na Musa. Alichukua govi la Gershomu na kulitupa miguuni pa Musa na kusema, "Wewe ni bwana arusi wa damu kwangu (Kutoka 4:25).

Ingawa hatuelezwi jibu la Musa lilivyokuwa kwa Sipora katika hali hii, wakati mwingine tunaposoma juu yake ni katika Kutoka 18. Hapa ilisomwa kwamba baada ya Musa kuwakomboa watu wa Israeli kutoka utumwani, Yethro alikuja kumtembelea akiwaleta. Sipora na wana wawili wa Musa walikuwa Gershomu na Eliezeri kwake. Kutoka 18:2 inatuambia kwamba Musa alikuwa amemrudisha mke wake kwa baba yake. Hatuambiwi hali za kurudi kwa Sipora kwa baba yake. Tunachojua ni kwamba alianza safari

pamoja na Musa wakiwa njiani kuelekea Misri lakini hakuwepo wakati aliwakomboa watu wake kutoka utumwani. Je, inawezekana kwamba jibu la Sipora kwa Musa katika suala hili la tohara ya mwana wao lilisababisha Musa kumpeleka nyumbani? Hatuambiwi.

